# صلاة العيد في المصلى هي السنة

## Mahali pa kuswalia ´iyd

Mtunzi:

Imaam, Faqiyh, ´Allaamah & Shaykh

Muhammad Naaswir-ud-Diyn al-Albaaniy

Tarjama: Firqatunnajia.com

# Yaliyomo

Dibaji ........ 3

Mtume daima aliswali ´iyd katika uwanja wa kuswalia ........ 10

Sunnah ni kuswali sehemu ya uwanja ........ 13

Hekima ya kuswali mahali pa uwanja ........ 23

Kuraddi shubuha ........ 28

# Dibaji

Himdi zote anastahiki Allaah. Tunamhimidi Yeye, kumtaka msaada na msamaha. Tunajilinde Kwake kutokana na shari ya nafsi zetu na uovu wa matendo yetu. Yule anayeongozwa na Allaah, basi hakuna awezae kumpoteza, na yule anayepotezwa na Allaah, basi hakuna awezae kumwongoza. Nashuhudia ya kwamba hakuna mungu wa haki isipokuwa Allaah na nashuhudia ya kwamba Muhammad ni mja na Mtume Wake.

Amma ba´d:

Kijitabu chetu cha leo ni chenye kuthibitisha ya kwamba Swalah ya ´Iyd Sunnah ni kuiswali katika uwanja wa kuswalia (مصلى) nje ya mji. Nilikuwa nimefikiria kukifanya kijitabu cha jumla kilichokusanya hukumu za Swalah ya ´Iyd kama jinsi nilivyofanya na "Swalaat-ut-Taraawiyh". Lakini kwa vile muda umekuwa mfinyu - kunabaki siku chache ´Iyd-ul-Fitwr ifike - nimedharurika kukifupisha. Hata hivyo ninataraji kuwa Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) atanisahilishia kukitoa kwa muda mfupi na kueneza kitabu kilicho cha jumla kitachoenezwa kwa watu. Kadhalika ninamuomba Allaah atukubalie kijitabu chetu kwa njia nzuri na pia waniombee katika du´aa zao za siri huenda - Allaah akitaka - akaninufaisha:

يَوْمَ لَا يَنفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ إِلَّا مَنْ أَتَى اللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ

“Siku ambayo hayatofaa mali wa watoto. Isipokuwa yule atakayefika kwa Allaah na moyo uliosalimika."[1]

[1] 26:88-89

Ndugu msomaji! Tambua ya kwamba mtunzi wa kijitabu "al-Iswaabah" ameandika kurasa mbili refu, uk. 14-15 kuhusiana na swalah ya ´Iyd sehemu ya uwanja ambapo wamejigonga wenyewe kwa njia ya kufedhehesha sana na imembainikia msomaji uchache wa elimu walionayo. Katika kitabu hicho wanatusemea uongo na kusema kwamba sisi hatuonelei kusihi kwa swalah ya ´iyd inayoswaliwa misikitini. Wamesema:

"Sababu iliyomfanya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuchagua kuswali mahali pa uwanja ilikuwa ni kwa sababu hakukuwepo nafasi yenye kutosheleza Madiynah al-Munawwarah kutokana na kwamba katika mji hapakuwa isipokuwa msikiti mmoja tu."

Huu ni ujinga uliyopindukia. Misikiti iliyokuwepo katika wakati wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ilikuwa ni mingi na inayojulikana. Miongoni mwa misikiti iliokuwa maarufu ni msikiti wa Qubaa´, msikiti wa Qiblatayn na msikiti wa Fath. Kumekuja Hadiyth nyingi Swahiyh katika vitabu vya Sunnah kuhusiana na misikiti hii. Haafidhw katika "Fath-ul-Majiyd" (01/455) ametaja kwa majina misikiti mingine na anaweza kurejea huko yule anayetaka.

Malengo yao kwa kuleta madai haya batili ni kutaka kuitokomeza Sunnah ya kuswali swalah ya ´Iyd uwanjani. Ndio maana wakawa wameleta sababu hii ya uongo kwamba Madiynah hapakuwa isipokuwa msikiti wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) tu. Isitoshe wanadai ya kwamba ulikuwa hauwatoshi waswalaji kuswali swalah ya ´Iyd! Lakini hata hivyo tumethibitisha ubatilifu wa sababu hii kwa kubatilisha madai kaunzia kwenye msingi wake. Hivyo basi tunasema endapo tukadirie kuwa msikiti wa Mtume ulikuwa hauwatoshi kuswali ndani yake, mtu anatakiwa kutambua kuwa kulikuwepo misikiti mingine mingi ambapo wangeliweza kuswalia, kama wafanyavyo watu hii leo. Kuacha kwao kuswalia ndani yake, na badala yake wakachagua kuswali uwanjani, ni dalili ya wazi kabisa yenye kuonesha kuwa Sunnah ni kuswali uwanjani pasi na misikiti. Makusudio yamethibitishwa na malengo yao ya utokomezaji yamebatilika.

Kisha wakasema:

"Wakati waislamu walipozidi kuwa wengi mpaka ikawa ni jambo lisilowezekana kwa waislamu kukusanyika sehemu ya uwanja, khaswa katika mji mkubwa kama Dameski, ndio wakakusanyika kwenye misikiti kutegemea na haja."

Ndugu msomaji, tazama mantiki hii iliyo kinyume! Wanasema kuwa kuwakusanya waislamu sehemu ya uwanja ni vigumu, wakati ukweli wa mambo ni kwamba ni jambo sahali na ni rahisi. Dalili yenye kuthibitisha hilo, ni kwamba miji mingi ilikuwa ni yenye

kufanya hivo, kama alivosema an-Nawawiy kwenye "Sharh Swahiyh Muslim". Himdi zote ni za Allaah kuona Sunnah hii mpaka hii leo inatendewa kazi katika miji mingi ya Kiislamu kama vile Dameski, Jordan, Misri, Algeria, Hijaaz, Pakistan na mingineyo.

Isitoshe kuna faida gani ya kufarikisha mkusanyiko wa waislamu kwa misikiti yote hii iliokaribiana, ambayo wakati mwingine mtu hupigi tambo khamsini kutoka kwenye msikiti mmoja hadi mwingine? Lau waandishi hawa wangeliyafungamanisha maneno yao kwa kuswali kwenye msikiti mmoja tu mkubwa, wangelikuwa na aliyewatangulia katika hili, kama itakavyokuja kuhusu Imaam ash-Shaafi´iy (Rahimahu Allaah). Lakini watu hawa wao hawaoni neno kusema kitu ambacho hakikusemwa na muislamu yeyote kabla yao pale wanapoipiga vita Sunnah. Vinginevyo waislamu wote wameafikiana juu ya kwamba Sunnah ni kuswali sehemu ya uwanja ikiwa msikiti haukuwatosha. Uhakika wa mambo ni kwamba wengi hawakukubali sharti hii, bali wamesema kuwa swalah inatakiwa kuswaliwa sehemu ya uwanja hata kama watapata nafasi ya kutosha msikitini. Kutokana na ujinga wao wamekwenda kinyume na waislamu wote, wale wa kale na wale waliokuja nyuma, ilihali Allaah (Ta´ala) amesema:

وَمَن يُشَاقِقِ الرَّسُولَ مِن بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ الْهُدَىٰ وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ الْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصْلِهِ جَهَنَّمَ ۖ وَسَاءَتْ مَصِيرًا

“Atakayempinga Mtume baada ya kuwa imekwishambainikia uongofu na akaifuata njia isiyokuwa ya waumini, basi Tutamgeuza alikogeukia na tutamwingiza Motoni - na uovu ulioje mahali pa kuishia!”[2]

Enyi watu, ala ala shikamaneni na Sunnah!

Kisha wakasema:

"... kwa sababu ya haja ya kitendo cha Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ndio maana aliswali msikitini kwa sababu ya udhuru."

Halafu wakaiwekea taaliki Hadiyth ya Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh) juu ya swalah yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) msikitini kwa sababu ya udhuru uliozuka wa mvua.

[2] 04:115

Hata Hadiyth ya Abu Hurayrah lau ikiwa kama imesihi, bado ni hoja yetu. Hata yenyewe kinachopata kufahamika ni kuwa lau isingelikuwa sio kwa sababu ya udhuru wa mvua angeliswali uwanjani. Hakuna waislamu wanaoenda kinyume na hili isipokuwa nyinyi peke yenu. Maneno yenu yaliyotangulia yanaashiria kuwa kuswali sehemu ya uwanja ni jambo halikuwekwa katika Shari´ah hii leo kwa sababu mnaonelea kuwa ni jambo lisilowezekana. Pamoja na hivyo tumewaraddi kwa Hadiyth ikawa ni hoja dhidi yenu na si hoja yenye kuwasapoti - na yote haya ni endapo Hadiyth yenyewe itakuwa ni Swahiyh. Uhakika wa mambo ni kuwa sio Swahiyh. Mlolongo wa wapokezi wake ni dhaifu, jambo ambalo tutalibainisha huko mbeleni.

Maneno yao mengine yasiyokuwa na maana hayastahiki kujibiwa. Isipokuwa tu maneno yao baada ya kunukuu Hadiyth ya kwanza yenye kutoka kwenye Hadiyth ya Abu Sa´iyd inayokuja na Abu Hurayrah:

"Faida tunayopata ni kwamba inasihi kuswali sehemu ya uwanja na pia msikitini na yote mawili kunapatikana thawabu ndani yake. Faida nyingine tunayopata katika Hadiyth ya kwanza ni kuwa lililo bora zaidi ni kuswali nje jangwani kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku zote alikuwa akilazimiana na hilo."

Ndugu msomaji! Tazama jinsi wanavyorudi katika haki ambayo sisi tunalingania kwayo! Kwa hayo wanayavunja maneno yao ya hapo kabla pamoja na sisi. Lakini hivi kweli unafikiria kuwa watabaki kuwa hivyo? Hapana! Hatimaye wamerudi kule walikoanzia na wakasema baada ya kunukuu maneno yafuatayo ya Imaam ash-Shaafi´iy yaliyonukuliwa na Haafidhw Ibn Hajar:

"Yule mwenye kutupia jicho Hadiyth ya al-Bukhaariy[3] iliyotangulia kutoka kwa Umm ´Atwiyyah:

“Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ametuamrisha kuwatoa katika [´Iyd] al-Fitwr na [´Iyd] al-Adhwhaa´; wanawali, wenye hedhi na wasichana mabikira. Ama wale wenye hedhi watajitenga na swalah.” Katika upokezi mwingine imekuja: “... uwanja wa kuswalia na watashuhudia kheri na ulinganizi wa waislamu.”[4]

[3] Ni kosa kumwegemezea Hadiyth hii al-Bukhaariy; ameipokea Muslim (3/20-21).

[4] al-Bukhaariy, Muslim na wengineo.

anapata kutambua kuwa sababu iliyopelekea Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kulazimiana siku zote kuswali sehemu ya uwanja ni ima msikiti wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakukuwepo nafasi ya wanaume na wanawake kwa siku mbili, au msikitini sio sehemu inayofaa kwa wanawake wenye hedhi."

Tumeyazingatia maneno yote haya na kuona kuwa hayana maana ni kama maneno yao mengine. Lau tutakubaliana nao kuwa msikiti wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakukuwepo nafasi yenye kuwatosha wanaume na wanawake wote, basi inatakiwa kutambulika kuwa hali kadhalika misikiti yetu hii leo. Hakuna msikiti hata mmoja ulio na nafasi ya kuwatosha waswaliji wote na hapo itabaki kuwa ni jambo limewekwa katika Shari´ah kutoka kwenda kuswali sehemu ya uwanja, jambo ambalo ndilo linalotakikana. Jengine ni kuwa ikiwa wao wanaonelea kuwa misikiti haifai kwa wanawake wenye hedhi kuhudhuria, basi ni lazima wakubali kuwa sehemu ya uwanja panawafaa. Wakilazimiana na kuswali misikitini, basi wamewakosesha kushuhudia mema na du´aa ya waislamu. Hili linaenda kinyume na kitendo cha Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika Hadiyth ambayo wao wanaiegemeza kwa al-Bukhaariy. Hadiyth ni moja katika dalili zetu zinazojulisha kuwa swalah inatakiwa iwe sehemu ya uwanja na sio msikitini. Pasi na kujali namna msikiti ulivyo mkubwa, ni jambo lisilowezekana kwa wanaume na wanawake wote wakapata nafasi ndani yake, jambo ambalo wao wamenyewe wamelikiri.

Moja miongoni mwa hoja zetu kwao ni pale waliposema:

"Wanawake, mpaka wenye hedhi, walikuwa wakitoka kwenda uwanjani na wakileta Takbiyr pamoja na Takbiyr zao."

Ni vipi mnaweza kuhakikisha Sunnah hii misikitini? Hamna njia ya kufanya hivo isipokuwa ikiwa kama mtawazuia kuhudhuria kabisa kabisa, jambo ambalo linaenda kinyume na kitendo chake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hata hivyo mnaweza kuwaamrisha kutoka na kubaki nje ya msikiti. Lakini vipi wataleta Takbiyr pamoja na waislamu wengine? Ndugu msomaji muislamu! Tazama namna ujinga unavyowafanya wenye nao na pata mazingatio!

**Uzindushi!**

Kutokana na yale tuliyonukuu, imepata kubainika kuwa waandishi hawa wanaonelea kuwa ni jambo limewekwa katika Shari´ah kwa kutoka kwenda katika uwanja. Yahifadhi haya. Huenda ikafika siku waandishi hawa kwa sababu ya hasadi na chuki wakapinga yale

ambayo siku moja walikuwa wakiyakubali pale watapoona wanusuraji wa Sunnah ni wenye kuitendea kazi Sunnah hiyo.

Sisi hata kama tunawahimiza wanawake kuhudhuria mkusanyiko pamoja na waislamu kwa ajili ya kuhakikisha maamrisho ya bwana wa Mitume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), haina maana ya kwamba tunapuuzia mavazi ya mwanamke yaliyowekwa katika Shari´ah. Haijuzu kwao kuonyesha kitu katika mwili wao isipokuwa uso na viganja vya mikono, jambo ambalo tumelifafanua katika kitabu "Hijaab-ul-Mar-ah al-Muslimah fiyl-Kitaab was-Sunnah". Allaah (Tabaarak wa Ta´ala) amesema:

يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُل لِّأَزْوَاجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَاءِ الْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِن جَلَابِيبِهِنَّ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰ أَن يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَيْنَ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا

"Ee Nabii! Waambie wake zako na mabinti zako - na wanawake wa waumini - wajiteremshie Jilbaab zao; hivyo kunapeleka karibu zaidi watambulikane wasiudhiwe. Na Allaah daima ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu."[5]

Pamoja na kwamba huko tumeweka wazi ya kwamba lililo bora zaidi ni kufunika uso na viganja vya mikono, tofauti na yale wanayoninasibishia baadhi ya waandishi ambao hawamchi Mola wa walimwengu.

Huenda baadhi wakashangazwa na wanawake kutoka kwenda kuswali swalah ya ´Iyd uwanjani. Basi itambulike kuwa kitendo hichi ndio cha haki kisichokuwa na shaka yoyote ndani yake kutokana na Hadiyth nyingi zilizopokelewa juu ya jambo hili. Kwa sasa tutatosheka na kutaja Hadiyth ya Umm ´Atwiyyah iliyotangulia ambayo haionyeshi tu dalili kuwa ni jambo limewekwa katika Shari´ah, bali ya kwamba ni wajibu. Kutokana na maamrisho yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na asli ya maamrisho yanaashiria uwajibu. Maoni hayo yanatiliwa nguvu na maneno ya Abu Bakr as-Swiddiyq ambaye amesema:

"Ni juu ya kila mwanamke mwenye shuka kutoka kwenda katika swalah za ´Iyd mbili."[6]

[5] 33:59

[6] Ibn Abiy Shaybah katika "al-Muswannaf" (02/184). Cheni ya wapokezi wake ni Swahiyh.

Je, mtu ambaye anadai kuwanusuru makhaliyfah waongofu anasema hivi pia? Wakati wa mwanzo wao ameamrisha jambo hilo. Hatukuwadhania hivyo. Hivyo ima wathibitishe kuwa tumekosea, jambo ambalo tunalipendelea zaidi, vinginevyo itawabainikia watu kikweli kile wanachomaanisha pindi wanapodai eti wanawanusuru.

Kusema ya kwamba kitendo hicho ni wajibu, ni jambo lenye kusapotiwa na as-Swan´aaniy katika "Subul-us-Salaam", ash-Shawkaaniy na Swiddiyq Hasan Khaan. Kadhalika ndio udhahiri wa maoni ya Ibn Hazm na ni kana kwamba Ibn Taymiyyah pia amemili kwayo katika "al-Ikhtiyaaraat" - na Allaah ndiye anajua zaidi.

# Mtume daima aliswali ´iyd katika uwanja wa kuswalia

Mahafidhi wahakiki wengi wametaja kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi sallam) siku zote alikuwa akiswali swalah ya ´Iyd sehemu ya uwanja[7]. Haya yanatiliwa nguvu na Hadiyth nyingi zilizipokelewa katika "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy na "as-Swahiyh" ya Muslim, vitabu vya Sunan na vya Musnad kupitia njia nyingi kabisa. Hivyo haina budi kutaja baadhi yake katika haraka hii ili ipate kumbainikia msomaji muheshimiwa ya kuwa niliyoyasema ndio ya sawa.

1- Abu Sa´iyd al-Khudriy (Radhiya Allaahu ´anh) amesema:

"Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akitoka siku ya Fitwr na siku ya Adhwhaa uwanjani[8]. Kitu cha kwanza alichokuwa akianza nacho ni swalah. Kisha akimaliza anawageukia watu waliokaa katika safu zao. Akiwapa mawaidha, kuwanasihi na kuwaamrisha. Ikiwa anataka kutuma kikosi, anafanya hivo[9], au kama akitaka kuamrisha kitu, basi anakiamrisha. Kisha anaondoka zake. Mpaka hii leo watu wanaendelea kufanya hivo."[10]

2- ´Abdullaah bin ´Umar (Radhiya Allaahu ´anhumaa) amesema:

---

[7] Tazama "Zaad-ul-Ma´aad" (01/172), "Fath-ul-Baariy" (02/361) na "Mukhtaswar Zaad-il-Ma´aad", uk. 44 ya Shaykh Muhammad bin ´Abdil-Wahhaab.

[8] Haafidhw amesema:

"Ni sehemu inayojulikana Madiynah iliyopo dhiraa elfumoja kutoka kwenye mlango wa msikiti."

Ibn-ul-Qayyim amesema:

"Ni uwanja wa kuswalia ambapo kunahifadhiwa mabegi ya mahujaji."

Inaonekana kana kwamba sehemu hiyo iko upande wa mashariki ya msikiti wa Mtume karibu na makaburi ya al-Baqi´, kama inavyofahamisha Hadiyth ya tatu.

[9] Hapa kuna ishara yenye nguvu ya kwamba Khutbah ya ´Iyd haikukomeka tu na mawaidha na maelekezo, bali ni ukumbusho na maelekezo yote yanayopelekea katika manufaa ya Ummah.

[10] al-Bukhaariy (02/259-260), Muslim (03(20), an-Nasaa´iy (01/234), al-Muhaamiliy katika "Kitaab-ul-´Iydayn" (02/86), Abu Nu´aym katika "al-Mustakhraj" (02/10/02) na al-Bayhaqiy katika "as-Sunan" (03/280).

"Siku ya ´Iyd alikuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) asubuhi na mapema akienda uwanjani, akiwa na mkuki ameubeba mbele ya mikono yake. Anapofika kwenye uwanja anausimika chini mbele yake. Halafu akiswali na kuuelekea, hilo ni kwa sababu sehemu ya uwanja ilikuwa wazi na kwa ajili hiyo hakukuwa na kitu cha kukielekea."[11]

3- al-Baraa´ bin ´Aazib amesema:

"Siku ya Adhwhaa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitoka kwenda Baqiy´[12] ambapo akaswali Rak´ah mbili. Kisha akatugeukia kwa uso wake na kusema: "Nusuuk yetu ya kwanza hii leo ni kuanza na swalah. Halafu tunarejea na kuchinja. Mwenye kufanya hivo, ameafikiana na Sunnah, na mwenye kuchinja kabla ya hapo, amefanya kitu alichoiharakishia familia yake na haina lolote haihusiani chochote na Nusuk."[13]

4- Kulisemwa kuambiwa Ibn ´Abbaas:

"Je, ulishuhudia ´Iyd pamoja na Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)?" Akasema: "Ndio, lau ingekuwa sio kwa sababu ya udogo wangu nisingefanya hivo. Aliswali alipofika katika bendera ilio karibu na nyumba ya Kathiyr bin as-Swalt. Kisha akatoa Khutbah na baadaye akawaendea wanawake akiwa pamoja na Bilaal. Akawapa mawaidha, akawakumbusha na akawaamrisha kutoa swadaqah. Niliona namna wanavyorusha [swadaqah] kwa pupa kwenye kanzu ya Bilaal. Halafu akaenda yeye na Bilaal nyumbani kwake."[14]

Muslim ameweka nyongeza katika upokezi wake kutoka kwa Ibn Jurayj:

[11] al-Bukhaariy (01/354), Muslim (02/55), Abu Daawuud (01/109), an-Nasaa´iy (01/232), Ibn Maajah (01/392) na Ahmad (6286). Tamko hili ni la Ibn Maajah na ndio yametimia na mlolongo wa wapokezi wake ni Swahiyh. Pia ameipokea al-Muhaamiliy (02/26-36), Abul-Qaasim ash-Shihaamiy katika "Tuhfat-ul-´Iyd" (14/16) na al-Bayhaqiy (03/284-285).

[12] Katika upokezi mwingine uwanjani.

[13] al-Bukhaariy (02/372) na tamko ni lake, Ahmad (04/282) na al-Muhaamiliy (02/90-96) na yale mapokezi mengine ni katika hizo mbili na mlolongo wa wapokezi wake ni mzuri.

[14] Ameipokea al-Bukhaariy (02/373) na tamko ni lake, Muslim (02/18-19), Ibn Abiy Shaybah (273/02), al-Muhaamiliy (38/39), al-Firyaabiy (85-93) na Abu Nu´aym katika "Mustakhraj" (02/08/2-9/01).

"Nilimwambia ´Atwaa´: "Je, hii leo Imaam ana haki ya kuwaendea wanawake na kuwapa mawaidha?" Akasema: "Ninaapa ya kwamba wana haki ya kufanya hivo. Na ni kwa nini hawafanyi hivo?."

## Sunnah ni kuswali sehemu ya uwanja

Ukishazitambua Hadiyth hizi basi hakika utaona kuwa ni hoja yenye kukata mizozo kabisa juu ya kwamba Sunnah ni kuswali swalah zote mbili za ´Iyd sehemu ya uwanja. Haya ndio maoni ya wanachuoni wengi. Imaam al-Baghawiy amesema katika "Sharh-us-Sunnah":

"Sunnah ni Imaam kutoka uwanjani. Ikiwa kutakuwa na udhuru wowote, basi ataswali mskitini."[15]

Msikiti ulioko ndani ya mji.

Imaam Muhyiy-ud-Diyn an-Nawawiy amesema katika pindi alipokuwa akizungumzia Hadiyth ya kwanza:

"Hii ni dalili kwa mwenye kusema kuwa imependekezwa kuswali swalah ya ´Iyd mahali pa uwanja na kwamba ni bora kuliko kufanya hivo msikitini. Kitendo hichi ndicho kinachofanywa na watu katika miji mingi. Kuhusiana na watu wa Makkah, walikuwa ni wenye kuiswali msikitini tangu hapo mwanzo. Wenzetu wana mitazamo miwili juu ya suala hili:

1- Bora ni kuswali jangwani, kutokana na Hadiyth hii.

2- Bora ni msikitini ikiwa hakuna kujibana. Maoni haya ndio sahihi zaidi kwa wengi. Wamesema kwamba sababu iliyowapelekea watu wa Makkah kuswali msikitini ni kutokana na upana wake na pia sababu ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) sehemu ya uwanja, ilikuwa ni kwa sababu msikitini kulikuwa na kujibana. Ni dalili inayofahamisha kuwa lililo bora ni kuswali msikitini ikiwa kuna sehemu ya kutosha."[16]

Hivi ndivo walivosema, lakini ni jambo linatakiwa kujadiliwa. Lau mambo yangelikuwa hivyo wanavyosema, basi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) asingelikuwa siku zote anaswali mahali pa uwanja, kwa sababu hakuwa ni mwenye kuendelea kulazimiana na jambo isipokuwa tu ikiwa kama ni kibora.

---

[15] Haya yamesemwa na Shaykh ´Aliy al-Qaariy katika "al-Mirqaat" (02/245). Tazama "Sharh-us-Sunnah" (04/294), al-Maktab al-Isaamiy kwa chapa ya Shu´ayb Arnaauutw kwa uhakiki wa Zuhayr ash-Shaawaysh.

[16] Sharh Swahiyh Muslim.

Kusema kuwa alifanya hivo kwa sababu ya kujibana kwa msikiti, ni madai yasiyokuwa na dalili yoyote. Linalotilia nguvu hilo ni kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akiswali swalah ya Ijumaa msikitini. Watu walikuwa wakija kutoka pande mbalimbali za Madiynah na kwenginepo na akiswali pamoja nao swalah ya Ijumaa ndani yake. Hakudhihiri tofauti yoyote kati ya idadi ya Maswahabaha wanaohudhuria swalah ya Ijumaa na idadi ya wanaokuja katika swalah za ´Iyd mpaka mtu aseme kwamba nafasi ilikuwa ni yenye kuwatosha wale na haiwatoshi hawa. Mwenye kudai kinyume na haya basi ni lazima kwake kuleta dalili, jambo ambalo sidhani kuwa analiweza.

Lau swalah za ´Iyd ingelikuwa ni bora kuziswali msikitini kuliko mahali pa uwanja na wakati huohuo msikiti kukawa na nafasi finyu, basi (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) angelikimbilia kuupanua kama walivyofanya baadhi ya makhaliyfah wake baada yake, jambo ambalo yeye alikuwa ana haki zaidi ya kulifanya kuliko wao. Ni jambo lisiloweza kufikiriwa kuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliacha kupanua baada ya kukubaliana na fadhila zilizotajwa. Isipokuwa hilo linaweza kukwepwa kwa kusema ya kwamba kulikuwepo kizuizi kilichofanya kusifanyike hilo, lakini sidhani kama kuna mwanachuoni anaweza kuthubutu kutamka madai kama hayo. Endapo atafanya hivo, tutakabiliana naye kwa maneno ya Allaah (Tabaarak wa Ta´ala):

هَاتُوا۟ بُرْهَانَكُمْ إِن كُنتُمْ صَادِقِينَ

"Leteni ushahidi wenu wa wazi mkiwa ni wakweli."[17]

Lililo la ajabu ni kuwa Shaafi´iyyah wameonelea kule Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku zote kuswali swalah ya Ijumaa kwenye msikiti mmoja ni dalili ya kutofaa kuswali swalah ya Ijumaa kwenye msikiti zaidi ya mmoja katika mji mmoja, na hawakufanya kule (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku zote kuswali swalah za ´Iyd mahali pa uwanja kuwa ni dalili ya kuwa bora zaidi ni kuziswali mahali pa uwanja kuliko msikitini. Kama unavyoona mwenyewe dalili ya mambo haya mawili ni moja. Haya yote yanatilia nguvu yale maoni ya kwanza ambayo yametajwa na Imaam an-Nawawiy (Rahimahu Allaah) na yako kwa wanachuoni wa Shaafi´iyyah. Haya pamoja na kuwa tofauti ilio kati ya hayo mawili ni ya rasmi na sio ya kiutenda kazi katika miji mikubwa kama Dameski, kwa sababu maoni ya pili yameweka wazi kuwa lililo bora zaidi ni kuswali msikitini kwa sharti waswaliji wote wapate nafasi. Tatizo ni kuwa misikiti kama hiyo

[17] 02:111

haipatikani. Katika hali hiyo kauli mbili hizo zinakutana, kama yalivyo maoni ya wanachuoni wengi, ya kwamba lililo bora zaidi ni kuswali mahali pa uwanja. Vilevile Imaam ash-Shaaafi´iy (Rahimahu Allaah) anaonelea kuwa imechukizwa kuswali msikitini ikiwa nafasi ni finyu, kama itakavyokuja huko mbeleni.

Haafidhw Ibn Hajar al-Asqalaaniy amesema chini ya Hadiyth ya kwanza:

"Hiyo imetumiwa kama dalili kuwa imependekezwa kutoka kwenda jangwa katika swalah ya ´Iyd na kwamba hilo ndio bora zaidi kuliko kuswali msikitini, kwa sababu Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku zote alikuwa akifanya hivo licha ya fadhila zinazopatikana katika msikiti wake. Imaam ash-Shaafi´iy amesema katika "al-Umm":

"Tumefikiwa na khabari ya kwamba Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akitoka kwenda mahali pa uwanja Madiynah katika swalah za ´Iyd na kadhalika yakafanywa na waliokuja baada yake. Udhuru uliokuwepo ilikuwa tu pale ambapo kunanyesha mvua au kitu kingine mfano wake. Kitendo hichi kinafanywa na watu wa miji yote isipokuwa tu Makkah."

Halafu akaashiria kuwa sababu ilikuwa ni kutokana na upana wa msikiti na ufinyu wa sehemu zilizoko nje ya Makkah. Amesema:

"Kama wakazi wa mji wana msikiti ambao watu wote wa mji watapata nafasi humo kwa ajili ya sikukuu, basi naonelea kuwa wasiuache. Hata hivyo ikiwa hakutokuwa nafasi ya kuwatosha, basi imechukizwa kuswali ndani yake na hivyo swalah isikaririwe."[18]

Kwa msemo mwingine ni kwamba sababu ni yenye kuzungukia ufinyu na upana, na sio kutoka kwenda jangwani. Lengo ni kutaka kuwafanya watu wote wawe kitu kimoja. Ikiwa hili litapatikana msikiti pamoja na ubora wake, itazingatiwa kuwa ni bora zaidi."[19]

Imaam ash-Shawkaaniy ameliwekea hilo taaliki na kusema (03/248):

"Hapa sababu inakuja kuwa ni "ufinyu na upana" ni jambo tu la kudhania lisilotilia nguvu udhuru wa kutomuigiliza (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kutoka kwenda kwenye jangwa baada ya kukiri kuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) siku zote alikuwa akifanya hivo. Ama kutumia hoja kwa kuswaliwa Makkah ya kwamba ndio sababu ya kutotoka

[18] al-Umm (01/207).

[19] Fath-ul-Baariy (02/450 - Salafiyyah)

kwenda jangwani, hilo linaraddiwa na uwezekano wa ufinyu kwa sehemu za nje ya Makkah, na sio kwa sababu msikiti wake haukukuwa na nafasi."

Uwezekano huu ambao umetajwa na Imaam ash-Shawkaaniy Imaam ash-Shaaafi´iy yeye mwenyewe ameuashiria, kama ambavyo punde kidogo nimetoka kunukuu kutoka kwa Haafidhw. Imaam ash-Shaafi´iy amesema:

"Nimesema haya kwa sababu hawakuwa na nafasi kubwa katika sehemu za nje ya Makkah."[20]

Haya yanatilia nguvu maoni ya ash-Shawkaaniy (Rahimahu Allaah) yaliyopo juu.

Inawezekana mtu akasapoti sababu hiyo kutokana na yale aliyopokea al-Bayhaqiy katika "as-Sunan al-Kubraa" (03/310) kupitia kwa Muhammad bin ´Abdil-´Aziyz bin ´Abdir-Rahmaan, kutoka kwa ´Uthmaan bin ´Abdir-Rahmaan at-Taymiy ambaye amesema:

"Katika uongozi wa Abaan bin ´Uthmaan Madiynah, usiku wa kuamkia siku ya Fitwr kulinyesha mvua kubwa. Akawakusanya watu msikitini na hakutoka kwenda mahali pa uwanja ambapo kulikuwa kukiswaliwa Fitwr na Adhwhaa." Kisha akasema kumwambia ´Abdullaah bin ´Aamir bin Rabiy´ah: "Simama na uwaeleze watu yale nimetoka kukueleza punde." ´Abdullaah bin ´Aamir akasema: "Wakati wa ´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anh) kulinyesha mvua kiasi cha kwamba watu hawakuweza kwenda mahali pa uwanja. Hivyo basi ´Umar akawakusanya watu msikitini na akawaswalisha. Halafu akasimama juu ya mimbari na kusema: "Enyi watu! Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akiwatoa watu kwenda mahali pa uwanja akiwaswalisha huko. Kwa sababu hivyo ndio kuzuri na kwenye wasaa na kwa kuwa msikiti haukuwa na nafasi yenye kuwatosha. Akasema: ”Kukinyesha mvua, basi bora ni kuswali msikitini.”[21]

Upokezi huu ni dhaifu sana. Muhammad bin ´Abdil-´Aziyz ndiye Muhammad bin ´Abdil-´Aziyz bin ´Umar bin ´Abdir-Rahmaan bin ´Awf al-Qaadhwiy. al-Bukhaariy amesema:

"Husimulia Hadiyth munkari."

an-Nasaa´iy amesema:

[20] al-Umm (01/207).

[21] as-Sunan al-Kubraa (3/310).

"Ni mwenye kuachwa."

Vilevile ash-Shaafi´iy ameipokea katika "al-Umm" (01/207) kupitia njia nyingine kutoka kwa Abaan bila ya Hadiyth kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kadhalika sababu hiyo imetokana na Swahabah na wakati huohuo mlolongo wa wapokezi wake ni dhaifu mno kwa sababu imetoka kwa mwalimu wa ash-Shaafi´iy ambaye ni Ibraahiym bin Muhammad bin Abiy Yahyaa al-Aslamiy alikuwa mwongo. Maalik amesema:

"Hakuwa ni mwaminifu katika Hadiyth wala katika dini yake."

Ndio maana Haafidhw amesema:

"Ni mwenye kuachwa."[22]

Kwa hivyo kusema kwamba sababu ilikuwa ni kutokana na ufinyu wa msikiti. Sambamba na hilo maoni ya wanachuoni yenye kusema kuwa Sunnah na jambo lililowekwa katika Shari´ah ni kuswali mahali pa uwanja katika kila zama na kila pahali, isipokuwa tu kukiwepo dharurah, yanabaki kuwa na nguvu. Simjui mwanachuoni yeyote ambaye elimu yake inategemewa aliyepingana na hili. Ibn Hazm amesema:

"Sunnah katika swalah za ´Iyd ni wakazi wa kijiji na mji watoke wende sehemu ya uwanja ilio wazi, katika pande za nje ya miji yao, asubuhi pale ambapo jua ni jeupe na inajuzu kuswali swalah za Sunnah."[23]

Halafu akasema:

"Ikiwa watapata uzito wa kutoka na kwenda mahali pa uwanja, basi waswali katika msikitini mkubwa."[24]

Kisha akasema:

"Imesimuliwa kwetu ya kwamba ´Umar na ´Uthmaan (Radhiya Allaahu ´anhumaa) waliwaongoza watu swalah ya ´Iyd msikitini kutokana na mvua iliyonyesha siku ya ´Iyd.

[22] at-Taqriyb.

[23] al-Muhallaa (05/81).

[24] al-Muhallaa (05/86).

Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akitoka na kwenda mahali pa uwanja kwa ajili ya kuswali swalah ya ´Iyd, jambo ambalo ndio bora zaidi. Hata hivyo mtu anapewa ujira kwa jengine pia, kwa sababu inahusiana na kitendo na sio maamrisho."[25]

Muheshimiwa Shaykh na Muhaddith kwa jina maarufu Ahmad Muhammad Shaakir ana utafiti mzuri na wenye kunufaisha kuhusiana na swalah ya ´Iyd mahali pa uwanja na kuhudhuria kwa wanawake. Napendelea nimnukuu kutokana na faida inayopatikana ndani yake. Amesema (Rahimahu Allaah):

"Je, hii leo Imaam ana haki ya kuwaendea wanawake na kuwapa mawaidha? Maoni ya wanachuoni juu ya suala hili ni mengi. ´Allaamah al-´Ayniy al-Hanafiy amesema baada ya Hadiyth ya Abu Sa´iyd (Radhiya Allaahu ´anh):

"Hadiyth inafahamisha kwamba mtu anatakiwa kwenda mahali pa uwanja na kusiswaliwe msikitini isipokuwa kwa dharurah tu. Ibn Ziyaad amepokea kutoka kwa Maalik ambaye amesema: "Sunnah ni kutoka kwenda katika jangwa isipokuwa kwa watu wa Makkah wanaotakiwa kubaki msikitini." [26]

Katika "al-Fataawaa al-Hindiyyah" imekuja:

"Kutoka kwenda kwenye jangwa kuswali swalah ya ´Iyd ndio Sunnah hata kama kutakuwa na nafasi ya kutosha katika msikiti mkubwa. Wanachuoni wako katika hili na ndio sahihi."[27]

Maalik anasema:

"Watu wasiswali swalah za ´Iyd sehemu mbili kama ambavyo vilevile hawatakiwi kuswali katika misikiti yao. Hata hivyo wanatakiwa kutoka kama jinsi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alivyokuwa akitoka. Ibn Wahb ameeleza kutoka kwa Yuunus kutoka kwa Ibn Shihaab ambaye amesema: "Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)

[25] al-Muhallaa (05/87).

[26] ´Umdat-ul-Qaariy (6/281-282).

[27] al-Fataawaa al-Hindiyyah (1/118).

alikuwa akitoka akienda mahali pa uwanja na baada ya hapo watu wengine wote wakaiga hilo."[28]

Ibn Qudaamah al-Hanbaliy amesema:

"Sunnah ni kuswali swalah ya ´Iyd mahali pa uwanja. ´Aliy (Radhiya Allaahu ´anh) aliamrisha hilo wakati al-Awzaa´iy na watu wa maoni wakaonelea kuwa ni jambo zuri. Kadhalika ndio maoni ya Ibn-ul-Mundhir. Kumesimuliwa kutoka kwa ash-Shaafi´iy kwamba anaonelea kuwa bora ni kuswali kwenye msikiti wa mji ikiwa ni mkubwa kwa sababu ndio sehemu bora na safi zaidi, na ndio maana watu wa Makkah wanaswali katika msikiti Mtukufu.

Kuhusu sisi, tunaona kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akitoka na kwenda mahali pa uwanja na anauacha msikiti wake. Vivyo hivyo ndio yaliyofanywa na makhaliyfah baada yake. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) haachi kitu kilicho bora zaidi pamoja na ukaribu wake na badala yake akajikalifisha kufanya kitu kilicho pungufu pamoja na umbali wake. Ni jambo halikuwekwa kwa Ummah wake kuacha kitu kilicho bora. Jengine ni kuwa sisi tumeamrishwa kumfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kumuigiliza. Ni jambo lisilowezekana kilichoamrishwa kikawa kina upungufu na kilichokatazwa kikawa ndio kikamilifu zaidi. Isitoshe haikupokelewa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba aliswali swalah ya ´Iyd msikitini isipokuwa kwa dharurah. Vilevile haya ndio maafikiano ya waislamu; siku zote na kila pahali wanatoka na kwenda mahali pa uwanja na kuswali swalah ya ´Iyd uwanjani hata kama msikiti utakuwa mpana au si mpana. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akiswali mahali pa uwanja pamoja na utukufu wa Msikiti wake."[29]

Ibn Qudaamah "Isitoshe haikupokelewa kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba aliswali swalah ya ´Iyd msikitini isipokuwa kwa dharurah... " anaashiria Hadiyth ya Abu Hurayrah (Radhiya Allaahu ´anh):

"Walipatwa na mvua siku ya ´Iyd ambapo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akawaswalisha msikitini."[30]

---

[28] al-Mudawwanah al-Kubraa (1/171).

[29] al-Mughniy (2/229-230).

[30] al-Haakim katika "al-Mustadrak" (1/295).

Ameipokea al-Haakim na imesahihishwa na adh-Dhahabiy[31].

Imaam ash-Shaafi´iy amesema:

"Tumefikiwa na khabari ya kuwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika swalah za ´Iyd alikuwa akitoka na kwenda mahali pa uwanja Madiynah na hali kadhalika yakafanywa na waliokuja baada yake. Kitendo hichi kinafanywa na watu wa miji yote isipokuwa Makkah. Hatukufikiwa na khabari yoyote kuwa kuna yeyote katika Salaf aliswali ´Iyd isipokuwa katika msikiti wao. Ninafikiri - na Allaah ndiye anajua zaidi - ya kuwa hilo ni kutokana na kwamba msikiti Mtukufu ndio sehemu bora kabisa duniani na kwa ajili hiyo ndio maana hawakupenda kuswali sehemu nyingine. Nimesema haya kwa sababu hawakuwa na nafasi kubwa sehemu za kando ya Makkah. Kadhalika sijui kuwa waliwahi kuswali ´Iyd wala swalah ya kuomba mvua pahala kwengine. Ikiwa wakazi wa mji wana msikiti ambapo watu wote wa mji watapata nafasi ndani yake kwa ajili ya sikukuu, basi naonelea kuwa wasiuache. Hata hivyo ikiwa hakutokuwa nafasi ya kuwatosha, basi imechukizwa kwa Imaam kuwaswalisha ndani yake na hivyo swalah isikaririwe.

[31] Kusema kuwa Hadiyth hii ni Swahiyh ni jambo linalohitajia kujadiliwa, kwa sababu ni yenye kuzunguka kwa ´Iysaa bin ´Abdil-A´laa bin Abiy Farwah ambaye amesikia kutoka kwa Abu Yahyaa ´Ubaydullaah at-Taymiy ambaye amesimulia kutoka kwa Abu Hurayrah. Vilevile imepokelewa na Abu Daawuud (01/180), Ibn Maajah (01/394) na al-Bayhaqiy (03/210). Cheni ya wapokezi hii ni dhaifu na haijulikani, kama alivyosema Haafidhw katika "at-Taqriyb". Isitoshe mwalimu wake Abu Yahyaa ´Ubaydullaah bin ´Abdillaah bin Mawhab ana hali isiyojulikana. adh-Dhahabiy amesema:

"´Ubaydullaah ni mdhaifu." (Mukhtaswar Sunan al-Bayhaqiy" (01/160/01))

Amesema pia juu yake:

"Anakaribia kutojulikana na Hadiyth yake ni munkari." (Miyzaan-ul-I´tidaal)

Kuafikiana kwake na al-Haakim juu ya kwamba ni Swahiyh katika "Talkhiysw al-Mustadrak", ni moja katika makosa yake mengi ambayo tunatarajia atasamehewa. Ndio maana Haafidhw amesema kwa kukata kabisa katika "Talkhiysw-ul-Habiyr", uk. 144, na "Buluugh-ul-Maraam" (02/99) ya kwamba mlolongo wa wapokezi ni dhaifu. Ndio maana maneno ya an-Nawawiy katika "al-Majmuu´" (05/05):

"Mlolongo wa wapokezi wake ni mzuri" (al-Majmuu´ (5/5))

si nzuri. Ni kana kwamba alitegemea kule Abu Daawuud kuinyamazia Hadiyth. Hata hivyo hili si lolote, kwa sababu Abu Daawuud mara nyingi hunyamazia mambo ambayo waziwazi ni dhaifu, jambo ambalo limetajwa katika vitabu vya isitilahi na kadhalika nimeyabainisha katika "Swahiyh Sunan Abiy Daawuud."

Kukinyesha au kukawepo udhuru mwengine, aswali msikitini na asitoke kwenda jangwani."[32]

´Allaamah Ibn-ul-Haajj amesema:

"Sunnah endelevu ni swalah za ´Iyd ziswaliwe sehemu ya uwanja. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Swalah moja katika msikiti wangu huu ni bora mara elfu moja kuliko misikiti mingine yote isipokuwa msikiti Mtakatifu. Swalah moja ndani yake ni bora mara laki kuliko misikiti mingine yote."[33]

Pamoja na fadhila zote hizi (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alitoka kwenda uwanjani kuuacha msikiti. Hii ni dalili ya wazi kabisa juu ya kwamba mtu anatakiwa kutoka kwenda mahali pa uwanja kuswali swalah za ´Iyd. Hii ndio Sunnah. Kuziswali misikitini ni Bid´ah kwa mujibu wa madhehebu ya Maalik (Rahimahu Allaah). Hata hivyo sio Bid´ah endapo kutakuwa na dharurah inayopelekea kufanya hivo. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakufanya hivo wala hakuna yeyote katika makhaliyfah zake waongofu baada yake aliyefanya hivo. Jengine ni kuwa (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliwaamrisha wanawake, kukiwemo wenye hedhi na wanawali, kutoka kwenda katika swalah za ´Iyd. Umm ´Atwiyyah (Radhiya Allaahu ´anh) alisema wakati Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipowaamrisha wanawake kutoka kwenda kuswali swalah ya ´Iyd:

"Ee Mtume wa Allaah, mmoja wetu hana Jilbaab." Akasema: "Dada yake ampe moja katika Jilbaab zake ili aweze kushuhudia mema na du´aa ya waislamu."[34]

Hivyo kukasunishwa swalah katika uwanja wa wazi ili kuonyesha desturi za Kiislamu."[35]

Sunnah ya kiutume iliyopokelewa katika Hadiyth Swahiyh inathibitisha kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akitoka na kwenda kuswali swalah za ´Iyd kwenye jangwa nje ya mji. Baada ya hapo waislamu wa mwanzo waliendelea kutendea kazi hili na hawakuwa wakiswali swalah za ´Iyd misikitini isipokuwa kukiwepo dharurah ya

[32] Kitaab-ul-Umm (1/207).

[33] al-Bukhaariy na Muslim.

[34] al-Bukhaariy na Muslim.

[35] al-Madkhal (283).

mvua na mfano wake. Haya ndio madhehebu ya maimamu wanne na maimamu wengine - Allaah awawie radhi.

Sijui yeyote aliyeenda kinyume na hili isipokuwa ash-Shaafi´iy (Radhiya Allaahu ´anh) ambaye anaonelea kuswali msikitini ikiwa kuna nafasi ya kuwatosha watu wote wa mji. Pamoja na hivyo haonelei kuwa kuna tatizo lolote kuswali jangwani hata kama kutakuwa nafasi ya kuwatosha msikitni. Vilevile ameweka wazi (Radhiya Allaahu ´anh) ya kwamba imechukizwa kuswali swalah za ´Iyd msikitini ikiwa kutakuwa hakuna nafasi ya kuwatosha watu wa mji.

Hadiyth zote hizi Swahiyh, kitendo cha kizazi cha mwanzo na maneno ya wanachuoni yanathibitisha kuwa ni Bid´ah kuswali swalah za ´Iyd misikitini. Yanaafikiana hata na maoni ya ash-Shaafi´iy, kwa sababu hakuna msikiti wowote katika miji yetu ambao unaweza kuwatosha watu wa mji wote."[36]

[36] Taaliki ya ´Allaamah Ahmad Shaakir juu ya "al-Jaamiy´" (2/421-424) ya at-Tirmidhiy.

## Hekima ya kuswali mahali pa uwanja

Sunnah hii tukufu ya kuswali kwenye jangwa ina hekima ilio kubwa na ya kina. Waislamu wana siku mbili kwa mwaka ambapo watu wa mji wote wanaume, wanawake na watoto wanakusanyika. Wanaelekea kwa Allaah kwa mioyo yao. Neno moja tu ndio lenye kuwakusanya. Wanaswali nyuma ya imamu mmoja. Wanasema "Allaahu Akbar" na "Laa ilaaha illa Allaah" na wanamuomba Allaah hali ya kuwa ni wenye kumtakasia nia. Ni kana kwamba wako katika moyo wa mtu mmoja; ni wenye furaha na kuburudika na neema za Allaah ambazo amewatunukia. Kwa hivyo sikukuu kwao inakuwa kweli ni sikukuu.

Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amewaamrisha wanawake wote kutoka kwenda kuswali swalah ya ´Iyd pamoja na wengine. Hakumbakiza yeyote na wala hakumpa udhuru mwanamke yoyote ambaye hakuwa na kitu cha kuvaa. Bali amemuamrisha aazime nguo kutoka kwa mwengine. Kadhalika amewaamrisha wanawake walio na udhuru wenye kuwazuia kuswali watoke wende mahali uwanjani ili washuhudie mema na du´aa ya waislamu.

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), makhaliyfah na viongozi manaibu walikuwa wakiwaswalisha watu swalah ya ´Iyd. Halafu wanawakhutubia, wanawawaidhi na wanawafunza mambo yenye faida na wao katika dini na dunia yao na kuwaamrisha kutoa swadaqah ili tajiri aweze kumuonea huruma masikini na yule masikini aweze kufurahikia fadhila za Allaah ambazo amemtunukia kutoka kwenye mkusanyiko huu uliobarikiwa wenye kushukiwa juu yake na rehema na radhi. Pengine waislamu wakaifuata Sunnah ya Mtume wao na wakazihuisha desturi za dini yao ambazo ndio msingi wa utatuzi na mafanikio yao:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اسْتَجِيبُواْ لِلّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُم لِمَا يُحْيِيكُمْ

"Enyi mlioamini! Muitikieni Allaah na Mtume anapokuiteni katika yale yenye kukupeni uhai."[37]

Shaykh Waliyyullaah ad-Dahlawiy amesema:

[37] 8:24

"Msingi wa hayo ni kwamba kila watu wana siku ambayo wanakusanyika na kutoka katika miji yao wakiwa wamependeza. Hii ni mila ambayo hakuna wasiokuwa nayo, ni mamoja waarabu na wasiokuwa waarabu. Wakati (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipofika Madiynah aliwakuta wanazo siku mbili ambazo wanacheza. Akasema:

"Allaah amewapa badali kwa zilizo bora zaidi; siku ya Adhwhaa na ya Fitwr."[38]

Imesemekana kuwa siku mbili hizi ilikuwa ni Nayruuz na Mahrajaan. Sababu ya kuzibadilisha ni kuwa hakuna sikukuu yoyote isipokuwa inakuwa na desturi fulani za kidini, imependekezwa na viongozi wa madhehebu au kitu mfano wake. Ndipo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akachelea endapo atawaacha na desturi zao kukahuishwa mambo mbalimbali ya sherehe za kikafiri au desturi za mababu zao. Ndipo zikabadilishwa kwa sherehe za imani ya upwekekaji iliosafi. Pamoja na kupendeza sikukuu mbili hizi zimekusanya pia kumdhukuru Allaah na ´ibaadah ili mkusanyiko wa waislamu usiwe peke yake na furaha pasi na kulinyanyua Neno la Allaah.

´Ibaadah ya kwanza ni siku wanayomaliza swawm na kutoa aina fulani ya zakaah. Hapa kunakusanyika furaha ya kimaumbile, kwa njia ya kwamba wanatua jambo lililowakuia ni gumu kwao na wakati huohuo fakiri anafurahikia zakaah, na furaha ya kubusara, kwa njia ya kufurahikia neema za Allaah alizowaneemesha kwa vile wamefuzu kutekeleza yale Aliyowafaradhishia na kuwaacha wakuu wa familia kubaki mpaka mwaka ujao.

´Ibaadah ya pili ni siku ambayo Ibraahiym alitaka kumchinja mwanae Ismaa´iyl (´alayhimaas-Salaam) ambapo Allaah akamkomboa kwa kumpa kichinjwa kitukufu. Hapa kuna mazingatio na mafunzo ya hali za viongozi wa dini ya upwekekaji ambao walijitolea maisha na mali zao kwa ajili ya kumtii Allaah. Kadhalika kuna makumbusho ya hajj pamoja na kutamani yale waliyomo. Ndio maana imesuniwa kusema "Allaahu Akbar". Amesema (Ta´ala):

وَلِتُكَبِّرُواْ اللَّهَ عَلَى مَا هَدَاكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

“Ili mumkabiri Allaah ambaye amekuongozeni.”[39]

[38] Ahmad na wengineo ikiwa na mlolongo wa wapokezi Swahiyh. Imetajwa katika "as-Swahiyhah" (2021).

[39] 2:185

Bi maana kushukuru kwa kukuwezesheni kufunga. Ndio maana imesuniwa kuchinja na kusema kwa sauti "Allaahu Akbar" siku za Minaa. Imependekezwa kutonyoa nywele kwa yule aliyenuia kuchinja[40]. Pia ni Sunnah kuswali na kutoa Khutbah ili mikusanyiko yao isikose kuwa na kumdhukuru Allaah na nembo za dini.

Ukiongeza katika haya ni kwamba malengo mengine ya Kishari´ah ambayo ni: kila Ummah unahitaji kuwa na sherehe ambapo watu wanakusanyika ili waonyeshe nguvu na wingi wao. Ndio maana imependekezwa kwa watu wote kutoka ikiwa ni pamoja vilevile na watoto, wanawake, wanawali na wenye hedhi ambao wanatakiwa kujitenga na mahali pa kuswalia na kushuhudia du´aa ya waislamu. Ndio maana Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikuwa akienda kwa kupita njia moja na mkurudi akipita nyingine ili njia zote mbili ziweze kuona nguvu za waislamu.

Ilipokuwa msingi wa ´Iyd ni mapambo, imependekezwa kuvaa nguo nzuri na kucheza dufu[41], kubadilisha njia na kutoka kwenda mahali pa uwanja."[42]

---

[40] Anaashiria maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Mtakapoona mwezi mwandamo wa Dhul-Hijjah na mmoja wenu akataka kuchinja, basi asikate kitu katika nywele zake wala kucha zake."

Katika upokezi mwingine imekuja:

"... asichukue kitu kutoka kwenye nywele zake wala kucha zake mpaka achinje kwanza." (Mukhtaswar Swahiyh Muslim (1251) na wengineo)

Udhahiri wa Hadiyth unafahamisha kwamba ni wajibu kuacha nywele na kucha kwa yule aliyenuia kuchinja mpaka atakapochinja. Kwa hivyo ni haramu kukata kitu katika hivyo vilivyotajwa. Haya ni maoni ya Imaam Ahmad na wengine. Wale waliopewa mtihani wa kunyoa ndevu wanatakiwa kulitia hili akilini. Kuna dhambi tatu katika kunyoa ndevu:

1- Kile kitendo chenyewe cha kunyoa ni cha kike, kuwaiga makafiri na ni kubadilsha maumbile ya Allaah. Haya nimeyabainisha katika kitabu changu "Aadaab-uz-Ziffaaf".

2- Kujipamba siku ya ´Iyd kwa kumuasi Allaah.

3- Hadiyth hii inafahamisha kuwa ni haramu kutoa nywele kwa yule anayetaka kuchinja. Uhakika wa mambo ni kwamba ni wachache wenye kusalimika na haya mpaka baadhi ya wanachuoni wametumbukia katika hayo - tunamuomba Allaah usalama!

[41] Anaashiria Hadiyth ambayo imepokelewa na Ibn Maajah (01/391) na wengineo kupitia sanadi mbili. Katika moja kuna Shariyk bin ´Abdillaah al-Qaadhwiy, ambaye hifdhi yake ni dhaifu, na nyingine mna Abu

Kutokana na yaliyobainishwa hapo mwanzoni umetambua kuwa Sunnah ni kuswali swalah za ´Iyd mahali pa uwanja na ni jambo ambalo maimamu wamekubaliana juu yake kutoka katika mtazamo wa kielimu. Vilevile kufanya hilo mahali pa uwanja kunapelekea katika faida na hekima nyingi ambazo hazipatikani kwenye misikiti mingi. Ndio maana inatakiwa kwa waislamu kurudi katika Sunnah ya Mtume wao (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kushirikiana na wale ambao wanapupia kuihuisha Sunnah hii katika miji hii. Hakika mkono wa Allaah uko juu ya kundi linalofuata Sunnah na sio kundi linaloenda kinyume nayo!

Haimstahikii mwenye busara kusema kwamba kuihuisha Sunnah hii kunapelekea kuwafarikisha waislamu, kwa sababu wakiswali katika misikiti yao makundi kwa makundi, kuswali mahali pa uwanja ina maana ya kwamba watatakiwa waiache na hivyo basi itakuwa ni kuzua makundi mapya - jambo tusilohitajia. Tuna haja ya kuyapunguza makundi, na sio kuyaongeza.

Haimpasi muislamu aliye na busara kusema maneno kama haya, kwa sababu yanapelekea katika matukio mabaya ambayo haiwezi kufikiriwa kuwa muumini anaweza kuyakusudia. Kwa maneno haya inapata kufahamika kuwa kuitendea kazi Sunnah na maoni waliokubaliana kwayo maimamu wote, jambo ambalo tumelibainisha kwa ufafanuzi, ni kuwafarikisha waislamu na kutawanyisha mkusanyiko wao. Kule kuyafikiria tu maneno haya kunatosheleza kubatilisha maneno haya. Uhakika wa mambo ni kwamba tunaona kuwa njia itayowafanya waislamu kuwa kitu kimoja ni pale wataporejea katika Sunnah. Hili ndilo tunamuabudu Allaah kwalo. Hili khaswa ile Sunnah ya kimatendo iliokuwa ikifanywa na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika maisha yake yote na akauacha juu yake Ummah wake na wengine waliokuja baada yake.

Ikiwa unataka kupata mfano wa karibu, basi inakutosheleza hali tuliyomo ya kuswali mahali penye uwanja. Waislamu leo wamefarikiana juu ya swalah hii na kugawanyika katika makundi mengi tofauti na Sunnah. Ikiwa tunataka kuwafanya wawe kitu kimoja, hatuna njia nyingine isipokuwa kutoka katika ardhi pana itayowakusanya waislamu wote wanawake kwa wanaume. Wafanye sehemu hii kuwa uwanja wa kuswalia na watekeleze hapo ´ibaadah hii kubwa, ambayo ni swalah ya ´Iyd. Haya ndio yaliyoamrishwa na Sunnah.

---

Ishaaq as-Sabi´iy ambaye alikuwa akichanganya mambo. at-Twahaawiy katika "Mushkil-ul-Aathaar (02/209-210) ameitia dosari kwa njia mbili tofauti. Anayetaka anaweza kurejea huko.

[42] Hujjatullaah al-Baalighah (2/30-31).

Vipi basi mtu anaweza kusema kuwa kuitendea kazi Sunnah hii kunafarikisha umoja wa waislamu!

Ndio, ni kweli ya kwamba kuihuisha Sunnah hii ina maana ya kwamba itapelekea kuunda mkusanyiko mpya na kuachana na ile mikusanyiko mingine iliyotawanyika inayofanyika kwenye misikiti mingi. Lakini pindi ilipokuwa makusudio ya mkusanyiko huu mpya ni kutaka kuikusanya mikusanyiko yote katika mkusanyiko mmoja, kama mambo yalivokuwa katika zama zake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na katika zama za makhaliyfah waongofu, ndipo ikalazimika kupatikana kwa mkusanyiko huu. Kwa sababu mkusanyiko mmoja hauwi kwa mara moja kama ambavyo hauwi pasi na wao. Isitoshe kuna msingi unaosema kwamba yale mambo ambayo yanahitajika ili kutekeleza jambo la wajibu basi nayo yatakuwa ni wajibu. Hili linazidi kuthibitisha zaidi utambuzi ya kwamba kuna udharurah wa kupatikana mkusanyiko mmoja huu, kwa sababu uko juu ya Sunnah ambayo malengo yake ni kuhakikisha mkusanyiko huu kwa maana yake pana tofauti na ile mikusanyiko mingine yote.

## Kuraddi shubuha

Huenda kukaja kikwazo kingine kwamba pengine watu wengi wenye nia nzuri wakaitikia mkusanyiko huu baada ya wao kubainikiwa na Sunnah. Lakini tatizo linakuja kuwa watu wengi watabaki ni wenye kugawanyika katika misikiti hii mingi kwa mujibu wa madhehebu tofauti na Sunnah. Kwa hivyo mkusanyiko huu mmoja hauwezi kuhakikishwa.

Ni kweli kuwa hili linaweza kutokea. Lakini ni jambo la wazi kabisa ya kwamba jukumu haliko juu ya wale walioihuisha Sunnah hii na kuwaita watu kwayo, bali ni kwa wale walioendelea kwenda kinyume nayo. Kwa hiyo wakemewe wao na si mwengine.

Ama kuhusu kundi la kwanza mkusanyiko wao ndio uliowekwa katika Shari´ah kwa sababu umejengeka juu ya Sunnah ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipokuwa akisifu Kundi Lililookoka:

"Ni Mkusanyiko."

Katika upokezi mwingine imekuja:

"Ni wale wenye kufuata yale niliyomo mimi hii leo na Maswahabah zangu."[43]

Hivyo basi hawatodhurika na wale wenye kwenda kinyume nao imgawa watakuwa ni wengi kuliko wao. Amesema (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Hakutoacha kuwepo kikundi katika Ummah wangu chenye kushinda juu ya haki. Hawatodhurika na wale wenye kuwakosesha nusura mpaka itapokuja amri ya Allaah na wao bado wako juu ya hayo."[44]

---

[43] Nzuri kupitia zengine. Imepokelewa na at-Tirmidhiy kupitia kwa ´Amr na ameifanya kuwa ni nzuri. Kadhalika imepokelewa na at-Twabaraaniy kupitia kwa Anas. Imetajwa pamoja na upokezi wa kwanza, ambao ni Swahiyh katika "Silsilah al-Ahaadiyth as-Swahiyhah" (204).

[44] Swahiyh na imepokelewa kwa mapokezi tele na ipo katika marejeo yaliyotangulia. Tazama "Mukhtaswar Swahiyh Muslim" (1095) na "Swahiyh al-Jaami´ as-Swaghiyr" (6177).

Muumini hatakiwi kujihisi upweke kwa sababu ya uchahe wa watu wenye kupita katika njia ya haki, kama ambavyo vilevile hadhuriki kwa idadi kubwa ya wapinzani. Imaam ash-Shaatwibiy amesema:

"Huu ndio mwenendo wa Allaah kwa viumbe; Watu wa haki ni wachache ukilinganisha na watu wa batili, hayo ni kutokana na maneno Yake (Ta´ala):

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ

"Wengi wa watu hawatoamini japokuwa utalipupa."[45]

وَقَلِيلٌ مِّنْ عِبَادِيَ الشَّكُورُ

"Lakini ni wachache sana miongoni mwa waja Wangu wenye kushukuru."[46]

Vilevile Allaah ataitimiza ahadi aliyomuahidi Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), nayo ni kwamba utarudi[47] kuwa kitu kigeni. Ugeni utakuwepo mpaka pale watu wake watakapotokomea au wakawa wachache. Hapo ni pale ambapo mema yatakuwa maovu na maovu yatakuwa mema na Sunnah ikawa ni Bid´ah na Bid´ah ikawa ni Sunnah. Yatapopitika hayo Ahl-us-Sunnah watakabiliwa na matusi na mashambulizi[48], kama jinsi ilivyokuwa mwanzoni wakikabiliwa na Ahl-ul-Bid´ah kwa matarajio ya kwamba wazushi wakusanyike katika upotevu. Lakini Allaah hataki wakusanyike mpaka kisimame

[45] 12:103

[46] 34:13

[47] Bi maana Uislamu. Anaashiria maneno yake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Uislamu ulianza hali ya kuwa ni mgeni na utarudi kuwa mgeni kama ulivyoanza – Twubaa kwa wageni!"

Ameipokea Muslim na wengineo. Imetajwa katika "as-Swahiyhah" (1273).

[48] Kama alivyofanya mtunzi wa "al-Iswaabah" baada ya kuchanganya mambo wakati alipokuwa akibainisha maoni yake juu ya swalah ya ´Iyd jangwani. Wamesema:

"Bado wapo waislamu wenye kuzihifadhi swalah zao na maamrisho ya dini yao. Baadaye kukaja kijikundi hichi kidogo na kikaanza kuwakaripia na kuwafarikisha."

Zingatia namna ambavyo wamefanya kulingania katika Sunnah ni jambo lenye kutenganisha mkusanyiko. Usirushie wengine mawe ikiwa nyumba yako wewe ni ya vio.

Qiyaamah. Mapote kamwe hayatokuwa na umoja juu ya wingi wao na kwa kuikhalifu kwao Sunnah. Bali kutaendelea daima kuwepo Ahl-us-Sunnah mpaka Qiyaamah kisimame. Pamoja na kuwa mapote mengi ya upotevu yanawachukia na kuwajengea uadui na bughudha ili wapate kukubaliana nao, bado ni wenye kuendelea kupambana ili wakubaliane nao, lakini bado ni wenye kuendelea kupambana, kuvutana na kuzuia mchana na usiku. Ndio maana Allaah anawaongezea ujira mwingi na kuwalipa thawabu kubwa."[49]

Ninamuomba Allaah (Ta´ala) atuthibitishe juu ya Sunnah na atufishe katika hali hiyo. Haya ndio ya mwisho yaliyonisahilikia kukusanya katika haraka hii - na himdi zote ni za Allaah, Mola wa walimwengu.

[49] al-I´tiswaam (1/12-13).